

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – The Story of Single Mothers in Africa”

EPISODE 5: “Who is responsible?”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: NIGHT IN THE COMPOUND

- **Drunkard Minabu (m, 55)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE TWO: NIGHT AT PAPA TILAHUN'S HOME

- **Papa Tilahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Drunkard Minabu (m, 55)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE THREE: AT NIGHT AT ASKALE'S HOME

- **Askale (f,21)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE FOUR:NIGHT AT PAPA TILAHUN'S HOME

- **Aster (f, 15)**
- **Narrator (m, around 35)**

INTRO:

Hamjambo, wapendwa wasikilizaji! Karibuni kwenye mchezo wetu wa redio wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Tujikumbushe baadhi ya matukio ya sehemu iliyopita: Begidu hajaonekana nyumbani kwa kiasi cha wiki moja tangu alipopigana na rafiki yake Samy, hakuna anayejua mahali alipo. Jonas ambaye ni ndugu mdogo wa Kassech akishirikiana na vijana wenzake, wameamua kumwibia Bwana Kasu, wala Jonas hajui kwamba huyo Kasu tajiri mkubwa ni babake! Hii ni sehemu ya tano, “ALAUMIWE NANI?” Tunaianza sehemu hii na kelele za mlevi Minabu akiwa kwenye uwanja wa nyumba yake, kwenye kitongoji cha jiji ambapo kisa hiki kinatokea.

SCENE ONE: NIGHT IN THE COMPOUND

1. SFX: NIGHT AMBIENCE, THUNDERS AND WIND

2. **Drunkard Minabu: (Monologue, speaks out aloud).** La hashu, Mimi siwaogopi nyinyi. Mnafikiri kwamba mlevi Minabu hayajui yote nyinyi mnayoyafanya sasa, usiku huu? **(Hiccups)** Najua, mnafurahia usiku pamoja na wake zenu **(laughs)**. Sijali hata kamwe! Nami pia amenifurahisha na nikampa busu la mwaka. **(Hiccup).**

Naam! Kipenzi changu, ebu nikubusu tena **(he drinks liquor from a bottle).**

KW Begin

Nyote mnajua fika kwamba ndimi pekee niliyesoma katika kitongoji hiki **(laughs)**. Hivyo basi, nisikilizeni kwa kituo; Nyinyi ni wavivu... **(Hiccup).**

3. SFX: THUNDERS AND WIND

4. Drunkard Minabu: Kwanza kabisa, mnapaswa kuisaka busara kama mimi! **(Laughs)**. Mtakapofanya hivyo mtaelewa vyema ninayoyasema. Naam, ni hatia kwenu nyinyi kujitumbuiza usiku bila kuyajali maishi ya baadaye ya watoto wenu! **(Drinks liquor from a bottle)** Si jambo linaloelekea katu! Kama una mtoto, unapaswa kujali maendeleo yake, tangu siku anapozaliwa. Je watoto wenu wanajihisi salama wawapo nyumbani? Mnavifahamu vipawa vyao na mambo yanayowatatiza? Mnahakikisha kwamba wana afya njema? Ebu niwaulizeni nyinyi watu, je mmewahi kuwasomea watoto wenu hadithi? Je mnawasaidia kufanya kazi za shule? **(Hiccup)** Mnapaswa kutumia muda wenu na nguvu zenu nyingi kuwatunza watoto wenu. **(Hiccup)**.

5. SFX: THUNDERS AND WIND

KW End

6. Drunkard Minabu: Mbona mimi ningali kapera? Bila shaka; kwa kuwa siwezi kuacha ulevi! **(Crying)** Hakuna mtu anayemhitaji mlevi! Mimi ni mlevi wa kutupa! **(Laughs)**. Kabla sijampata mtoto, sina budi kuzingatia iwapo nitampa malezi bora. Sitaki kuandamana naye kwenye baa tukanywe pombe pamoja! Hapana, hapana, hapana, hapana! **(Hiccup)** Ninawaambia, watunzeni watoto wenu!

7. SFX: HEAVY RAIN

8. NARRATOR: Kama kawaida, wazee wenye nyumba, Papa Tilahun na Mama Beletu, wanamchungulia mlevi kupitia dirishani. Wanaamini kwamba huyo mlevi aghalabu asemayo yana ukweli kiasi fulani. Mlevi anakabiliwa na mvua kubwa na anajaribu kujimakini. Miguu yake inatetemeka.

SCENE TWO: NIGHT AT PAPA TILAHUN'S HOME

9. SFX: HEAVY RAIN OUTSIDE

10. Minabu: **(Shouts from outside)** Napenda watoto.
(Drinks liquor from a bottle) Nampenda jirani yangu Kassech na mwanawe! Maskini Begidu, juma limeshakwisha wala hakuna anayejua uliko! Maskini! **(Cries)**. Maskini Kassech! **(He**

throws the bottle away).

11. SFX: SMASHING BOTTLE

12. Papa Tilahun: **(while he looks through the window)** Mama Beletu muone, ameigongesha chupa yake ukutani! Umesikia alivyosema?

13. Mama Beletu: Nimesikia kila alailolisema.

14. Papa Tilahun: Huyu mlevi Minabu asemayo ni kweli!

15. Mama Beletu: Nilishakwambia tangu kitambo kwamba huyo ni mtu na elimu yake. Halafu, sasa ni zamu yangu kuchungulia. Ebu nione anayofanya huko nje. **(Pause)**. Anapepesuka mvuani.

KW beign

16. Papa Tilahun: Maskini! Minabu, ni mtu aliyechanganyikiwa. Amezoea kutukana majirani zake kila usiku lakini ikifika asubuhi siku ya pili hakumbuki lolote ...

17. MINABU: **(From outside, loudly)** Ninawambieni ukweli; Simwogopi Papa Tilahun!

18. Mama Beletu: **(Laughs).**

19. Papa Tilahun: Usiyazingatie anayoyasema. Kesho asubuhi na mapema atatubishia mlango kukutaka radhi kama kawaida yake.

20. Mama Beletu: **(Exited)** Anapepesuka kuja huku tuliko!

21. Papa Tilahun: Ebu nione!

KW end

22. SFX: BANGS, AS SOMEONE FALLING DOWN IN THE MUD

23. Mama Beletu: Subiri! Masikini! Ameanguka.

24. Papa Tilahun: Harakisha! Fungua mlango. Ni lazima tumsaidie.

25. SFX: DOOR OPENING

26. SFX: HEAVY RAIN GETS LOUDER

27. NARRATOR: Wakati Papa Tilahun na Mama Beletu wanapokwenda kumsaidia Minabu; Askale, akiwa nyumbani kwake, anamfariji rafiki yake Kassech, ambaye mtoto wake ametoweka. Mwanawe Askale, Samy ameshalala.

SCENE THREE: AT NIGHT AT ASKALE’S HOME

28. SFX: HEAVY RAIN OUTSIDE, DRUNKARD SCREAMS IN BACKGROUND

29. Kassech: (Sobbing).

30. Askale: Kwa hisani yako, usilie Kassech; Usikate tamaa.

31. Kassech: Askale niambie tutampata wapi Askale?
(Cries) Juma moja limepita tangu alipotoweka lakini hakuna mtu ambaye amemuona. Nitampata vipi? Nimejitahidi vya kutosha lakini nimeambulia patupu. **(In agony)** Maskini, mtoto wangu! Mwanangu! Uko wapi katika baridi hii yote? **(cries).**

32. Askale: Mwenzangu, usilie, tafadhali.

33. Kassech: **(Cries more)** Nalia nikilia! Mimi ndiye wa kulaumiwa. Lau kama nilifuata ushauri wako, nisingempoteza mwanangu. Najilaumu mimi! Lawama kwangu mimi! **(cries)**

34. Askale: Mimi ni mama na ninaelewa vyema unavyohisi.

Najua unaumia kwa kiasi kikubwa. Lakini hata ukilia, kilio chako kitamrejsha Begidu?

(Pause) Hapana!

35. Kassech: **(Sorrowfully)** Sina raha hata kidogo, ninajihisi mpweke. Nina dhiki si kidogo! **(Pause then firmly)** Umesema kweli, kulia hakusaidii chochote. Mimi ndiye niliyesababisha mwanangu atoweke!

36. SFX: HEAVY RAIN OUTSIDE TURNS INTO DRIZZLING

37. Askale: Ninaamini; utampata!

38. Kassech: Na nikimpata mwanangu nitajitahidi kumtendea vyema. Ninakuahidi, Askale, nitampenda kwa dhati. Kumtukana na kumpiga mtoto si jambo zuri; asema Minabu huko nje ni kweli. Mwanao ana bahati sana, Askale!

39. Askale: Wajua, watoto wanahitaji kupendwa kama wanavyohitaji chakula na vinywaji. Unapaswa kutumia muda wako mwingi na mwanao. Anakuhitaji. Akitenda jambo zuri, huna budi kumsifu. Hata akitenda jambo lisiloelekea, usimtukane wala kumpiga, bali umweleze kosa lake na jinsi ya kujirekebisha. Watoto ni wepesi wa kuelewa mambo. Watoto wanatakikana

kujihisi salama wakiwa nyumbani. Lakini Begidu anaogopa kila kitu. Ndiyo sababu akakimbia nyumbani. Atakaporudi kaa naye kwa mapenzi.

40. Kassech: **(Sorrowfully)** Nitafanya hivyo, nitafanya hivyo...pale nitakapompata...

41. Askale: Utafanya hivyo! Kweli. Na pia jambo jingine muhimu, jaribu kumsaidia kufanya kazi za shule, na kabla hajenda kulala msimulie hadithi, au umwimbie wimbo anaoupenda.

42. SFX: RAIN STOP

KW BEGIN

43. Kassech: Unanishangaza sana! Hayo yote uliyajuaje? Sote tulisoma shule moja, lakini unajua mambo mengi zaidi yangu mimi.

44. Askale: Ndiyo sababu ninakusumbua mara kwa mara nikikwambia urudi tena kwenye masomo ya jioni **(Laughs)**.

45. Kassech: **(Laughs)** Hapana, hujanisumbua, vinginevyo umejitahidi kunishauri lakini mimi sikuufuata ushauri wako.

46. Askale: Hujachelewa hata kidogo. Anza masomo yako

ya usiku mara moja. Wajua, mara nyingine hubaki darasani nikizungumza na walimu kuhusu jinsi ya kuwapa malezi mema watoto wetu. Wote wana watoto wa kiume na kike na wanajua jinsi kusimamia kazi zao, familia zao na pia kujiendeleza kimasomo. Kwa kweli wamenifaa sana.

47. Kassech:

Sijawa na makini!

48. Askale:

Wajua, kuna vitu vingi ambavyo tunaweza kuwafanyia watoto wetu bila kutumia hata shilingi moja. Kwa mfano, nakujua wewe una ujuzi wa kusimulia hadithi. Unaweza kumhadithia Begidu visa bila gharama na mwanao atajifunza mengi kutokana na hilo.

49. Kassech:

Kweli!

50. Askale:

Akikuuliza suali lolote, usimkatize bali jaribu kumjibu kiasi cha uwezo wako. Basi rafiki yangu, ikiwa unataka kujifunza zaidi, kwa hisani yako rudi tena masomoni.

51. Kassech:

Ninatoa ahadi kwako! Nikimpata mwanangu, nitaanza masomo mara moja. Kwanza nimpate Begidu, kisha ninatakikana kufanya kazi kwa bidii ili nipate fedha za kugharamia masomo yangu. Natumai kuwa pia mdogo wangu Jonas

atarejea nyumbani hivi karibuni>

52. Askale: Natumai hivyo pia!

KW END

53. Kassech: Haya, mvua imekatika. Naomba niondoke
sasa.

KW begin

54. Askale: Mbona? Tafadhali kaa kidogo. Acha nikuletee
chakula.

55. Kassech: La, la, la, asante sana, Askale! Nataka nifike
nyumbani kabla mvua haijaanza tena. Hali ya
hewa inashangaza. Mvua haitabiriki **(Walks)**.

KW end

56. Askale: Haya! Usijali!

57. Kassech: Sawa. Lala salama!

58. Askale: Lala salama!

59. SFX: DOOR OPENS

60. SFX: DOOR CLOSES

61. NARRATOR: Kassech anajilaumu kwa tabia yake. Hata hivyo,

mazungumzo ya leo kati yake na Askale yamemfanya kumakinika. Kina mama hao wawili walikuwa na ugomvi mkubwa baada ya watoto wao kupigana. Leo ndio mara ya kwanza ambapo Kassech amezungumza na rafiki yake tangu Begidu alipotoweka. Wakati huo huo, Papa Tilahun na mkewe wamemsindikiza Minabu chumbani kwake. Aster, mjukuu wa Papa Tilahuni na mkewe yuko nyumbani. Amekuwa akizungumza kwa simu na rafiki yake wa dhati Semira.

SCENE FOUR: NIGHT AT PAPA TILAHUN'S HOME

62. SFX: NIGHT AMBIENCE

63. Aster: **(Monologue on the phone)** Una hakika Semira kwamba huyo ni mpwa wa Jonas? ... Kweli?! Siamini ... **(laughs joyfully)** Najua Semira, wewe ni rafiki yangu wa dhati. ... **(Suspicious)** Lakini nini ...? Nini? Semira, una hakika ni Begidu? ... Siamini. **(shocked)** Maskini! Yarabi! Wapi ...! **(Cries)** Nitamwambiaje mama yake? ... Nitakupigia simu kesho liwe liwalo, Semira, asante.

64. SFX: HANGS UP THE PHONE

65. Aster: **(Sobs).**

66. SFX: NIGHT AMBIENCE

OUTRO:

Kwani Aster ameambiwa nini na rafiki Semira kwenye mazungumzo yao ya simu? Mbona Aster ameshtuka sana hivyo? Je Kassech atafanikiwa kumpata mwanawe kama rafikiye Askale anavyotumai, ama tayari ashachelewa? Sikiliza kipindi chetu kijacho. Unakaribishwa kuchangia mawazo na mapendekezo yako kuhusu ulezi wa watoto wadogo. Pia unaweza kufungua ukurasa wetu wa tovuti: dw.de/lbe. Hadi tutakapokutana tena – kwaheri!